"Tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu." (Acts 2:38)

CENTER FOR JAIL TRANSFORMATION

"Kwa maana mkiwasamehe watu makosa yao, na Baba yenu wa mbinguni atawasamehe ninyi.Bali msipowasamehe watu makosa yao, wala Baba yenu hatawasamehe ninyi makosa yenu." (Matt. 6:14-15)

KUMFUATA YESU KUELEKEA UHURU

YESU ALISEMA, **"NIFUATE"** MARA 13 KATIKA INJILI – HILI LAZIMA LIWE MUHIMU, SAWA?

1. ***MSAADA***
   Wakati unapokuwa tu ndo umeianza safari yako ya kumfuata Yesu, inasaidia sana ukipata msaada. Kama inawezekana, jiunge na kikundi cha kujisomea biblia, kikundi cha maombi au angalau tu kutana na wafuasi wengine wa Yesu 2 au 3 ambao wamekuwa wafuasi muda mrefu kuliko wewe. Usiogope kuomba msaada kwa kadiri unavyoendelea kukua katika imani yako – hivyo ndivyo Yesu alivyoweka iwe.

2. ***BIBLIA – NENO LA MUNGU***
   Je, unafahamu kwamba moja ya majina ya Yesu katika Biblia ni "Neno la Mungu"? Unahitaji kuwa na Biblia yako binafsi, kwa sababu ni Neno lake Mungu mwenyewe kabisa! Tunapendekeza kwamba upate toleo ambalo ni rahisi kusoma na kuelewa (baadhi ya matoleo maarufu ya Kiingereza ni NASB – New American Standard Bible, the NIV – New International Version, or the ESV – English Standard Version). Muombe Mchungaji wa gerezani kwako, Mhudumu anayejitolea kuja kuleta huduma hapo gerezani, au ndugu mwanafamilia akupatie moja.

3. ***BATIZWA***
   Yesu aliwambia wanafunzi wake (na sisi) kwamba mara tu tunapokuwa watu wanaoamini katika Yeye na kuchagua kumfuata Yeye kama Bwana wetu, tunahitaji kubatizwa katika maji kuonesha hilo badiliko katika maisha yetu. Kama unaweza kubatizwa mahali ambapo unaishi sasa, fanya hivyo. Kama unahitaji kusubiri mpaka baadaye, hakikisha unafanya hivyo pale tu utakapopata fursa yako ya kwanza!

4. ***ANZA KUSOMA BIBLIA YAKO***
   Kama unahitaji mahali pazuri pa kuanzia, tunapendekeza uanzie Injili ya Yohana. Inakubalika na wengi kuwa ni sehemu nzuri sana ya Biblia kwa wale wanaoanza. Inakupasa uweke lengo la kusoma angalau dakika kwa 10 kila asubuhi au kwa kadiri ratiba yako itakavyokuwa inaruhusu. Kufanya hivyo kila siku kutasaidia kufanya usomaji wa Biblia kuwa tabia ya kudumu maishani.

5. ***ANZA KUOMBA***
   Mwombe Bwana akusaidie kuongea naye na kuisikia sauti yake kadiri anavyokuongoza na kujibu maswali yako. Maombi hayahitaji kuwa kitu cha ajabu au kitu kigumu sana. Ni rahisi kama vile kuongea na rafiki yako. Moja ya maombi bora ya kuanza nayo ni kuomba, "Bwana, sitaki kuyarudia maisha yangu ya zamani. Nataka yote uliyonayo kwa ajili yangu. Nijaze uzima wako mpya na nipe nguvu ya kuishi kwa ajili yako kila siku." Inakupasa uweke lengo la kuomba angalau kwa dakika kwa 10 kila asubuhi au kwa kadiri ratiba yako inavyoruhusu.

6. ***NENDA KANISANI***
   Moja ya desturi muhimu ya mfuasi wa Yesu ni kumwabudu Yeye kila wiki pamoja na jamii ya waaminio katika eneo lako unaloishi. Mara nyingi, hii ni ibada ya Kikanisa ya Jumapili asubuhi mahali pa kufanyia ibada. Au inaweza kufanyika kwa namna nyingine, inategemea mazingira yako. Lakini Yesu aliweka bayana kabisa kwamba tunahitaji kuunda jamii ya wafuasi waaminifu na kujitahidi kuoneshana pendo lake sisi kwa sisi, na kwa ulimwengu unaopotea na kuangamia.

7. ***WAAMBIE WENGINE KILE AMBACHO YESU AMEFANYA KWENYE MAISHA YAKO***
   Mara nyingi huitwa "kushuhudia" au "kuwambia wengine ushuhuda wako", ni sehemu muhimu ya maisha yako mapya (ndani ya Kristo) kushuhudia, kwa namna iliyo rahisi na ya kirafiki, jinsi ambavyo Yesu amebadilisha maisha yako. Umekuwa mtu aliyebadilika sasa kwa sababu mmoja wa wafuasi wa Yesu alikuja mahali unapoishi na akakushuhudia habari njema kuhusu ushuhuda wake. Wewe pia imekupasa kufanya hivyo.

8. ***ISHI AINA YA MAISHA YA YESU***
   Yesu anatuita sio tu "kwenda kanisani" na "kuwa mtu mzuri" bali tujifunze kumwacha yeye aishi maisha Yake kupitia sisi ili kusaidia kuponya na kuokoa ulimwengu ulioharibika. Njia kuu tunayotumia kufanya hivyo ni kukutana pamoja kila wiki na watu wenye nia kama hiyo (mara nyingi huitwa "wanafunzi") na tunashirikishana mapito ya maisha, tunaombeana, tunatiana moyo, na kuona kila mmoja wetu anakua katika Bwana. Tunaporuhusu nuru ya Bwana iangaze kutokea ndani yetu, waamini wengine na watu wasiomwamini watavutwa kuja Kwake. Yeye alituambia, "Ninyi ni nuru ya Ulimwengu. Nuru yenu sharti iangaze mbele za watu kiasi ambacho watayaona matendo yenu mema, na wamtukuze Baba yenu aliye mbinguni. " Mwamini Mungu na tarajia mambo makubwa!

Kwa hiyo, tunaelekea wapi na yote haya? Tunaelekea mahali panapoitwa UHURU. Kama umefungwa kwenye eneo lolote la maisha yako, hizi hapa ni baadhi ya hatua za kumfuata Yesu kuelekea uhuru kamili, hata kama utabaki gerezani kwa miaka mingi ijayo.

- Mwombe Bwana atawale maisha yako; mwamini Yeye kukupa mahitaji yako, kuwa Mfalme wako, kuwa rafiki yako, kuwa chanzo chako cha nguvu zako na mponyaji wako.
- Mwombe akuweke huru mbali na kila tabia zote zisizompendeza au zinazokuzuia kumfuata kwa uhuru. Kuwa tayari kubadilika!
- Yesu anaye adui: Ibilisi au Shetani. Unapochagua kumfuata Yesu, Ibilisi anakuwa adui yako pia. Mwombe Yesu akulinde na kukuokoa na kila kazi mbaya za Ibilisi.
- Mwombe Yesu akuponye kila maumivu na majeraha yote ya mambo ya maisha yako yaliyopita au mapito yako. Kadiri unavyotumia muda mwingi naye katika maombi, faragha, na kusoma Neno lake, Biblia, ndivyo utakavyokuwa huru zaidi!

UNAWEZA UKAISHI UKIWA HURU KIROHO, KIHISIA, NA KIAKILI HATA UKIWA BADO UPO GEREZANI!

"YEYE AMBAYE MWANA AMWEKA HURU YU HURU KWELI KWELI." (John 8:36)

Mpango wa Biblia kwa mwanafunzi wa kweli ni mtu anayefanya wanafunzi ambaye huenda tena na kufanya wanafunzi zaidi. Hili ni jambo la kufanya mfuasi wa Yesu maisha. Anasema katika Mathayo 28:19 "Enendeni na mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi."

Kumbuka: Haufanyi mambo haya ili kumfanya Yesus akuokoe. Unayafanya kwa sababu tayari amekwishakuokoa!

Ifuatayo ni baadhi ya mistari ya Biblia inayothibitisha na kufafanua mambo yaliyotajwa hapo juu:

1. 1 Wathesalonike 5:11, Waebrania 10:24-25; Mhubiri 4:9-12; Mithali 27:17; Mathayo 18:20; Wakolosai 3:16
2. Yohana 1:1, Ufunuo 19:13; 2 Timotheo 3:16-17; Mathayo 7:24; Mathayo 4:4; Zaburi 33:4; 1 Petro 1:23 & 2:2
3. Mathayo 28:19-2; Marko 16:16; Matendo ya Mitume 2:38, 10:47, 19:5; Warumi 6:3-4
4. Yoshua 1:8; Zaburi 119:105; Warumi 15:4; Zaburi 119:11; Waebrania 4:12; 2 Timotheo 2:15; Zaburi 119:9
5. Marko 11:24; Warumi 12:12; Wakolosai 4:2; Wafilipi 4:6-7; 1 Wathesalonike 5:16-18; 1 Yohana 5:14
6. Matendo ya Mitume 2:42 & 9:31; Warumi 12:4-5; Waefeso 4:14-16 Waebrania 10:24-25
7. Mathayo 5:16; 2 Timotheo 1:8 & 4:2; 1 Petro 3:16-17; Wakolosai 4:5-6
8. Mathayo 4:19-20 & 28:19-20; Yohana 1:45; Warumi 10:14–15; 2 Timotheo 2:2

Tunataka kutoa shukrani za kipekee kwa *Think Twice Ministries* pamoja na kwa ndugu Guy & John Earle, walio-changia kuandikwa jarida hili.

JAMBO LA KUZINGATIA KWA WANAOJITOLEA KUHUDUMU GEREZANI

Bila shaka, mtu ambaye ni mpya au ndo kwanza anaanza kumfuata Kristo ataendelea vizuri na kukua kwa haraka kama ana mtu wa kumtia moyo na kutembea pamoja naye. Ongeza urafiki wako katika hatua hizi na tazama muujiza ukiten-deka!

JAMBO LA KUZINGATIA KWA WACHUNGAJI WA GEREZANI

Mwongozo huu umetayarishwa mahususi kwa mazingira yale ambayo tukio la uinjilisti limefanyika na watu waliopo gerezani au Jela wakamwamini Yesu, hasa kwa mara ya kwanza.Tumia huu "Mwongozo" kuwapa mwelekeo wa kivitendo wa kuwasaidia kukua,hata kama wako katika mazingira ya kukaa peke yao au hali ya kutengwa. Upakue kwenye tovuti hii **www.LoveYourJail.com**. Majarida mengine ya bure yanapatikana humo pia.

Jarida hili halina hatimiliki. Jisikie huru kutoa nakala na kusambaza kwa kadiri ya uhitaji.